

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU
HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA WAKATI WA HAFLA YA UZINDUZI WA
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (PDPC),
UKUMBI WA JNICC, DAR ES SALAAM,
TAREHE 03 APRILI 2024**

*Mheshimiwa Nape Moses Nnauye (Mb.), Waziri wa Habari,
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;*

Wahshimiwa Marwaziri na Naibu Marwaziri mliopo;

Mwakilishi wa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;

*Mheshimiwa Selemani Kakoso (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati
ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;*

*Mheshimiwa Suleimani Zedi (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya
Kudumu ya Bunge ya Katiba, Utawala na Sheria;*

*Bwana Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu wa Wizara
ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;*

*Dkt Suleiman Mdewa, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi,
Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi ya
Zanzibar;*

*Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es
Salaam;*

*Mheshimiwa Balози Adadi Mohammed Rajabu; Mwenyekiti wa
Bodi ya Wakurugenzi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;*

Mheshimiwa Bi. Fatma Mohammed Ali, Makamu Mwenyekiti

Bodi ya Wakurugenzi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

Ndugu Emmanuel Lameck Mkilia, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

Ndugu Nehemiah Mchechu, Msajili wa Hazina;

Waheshimiwa Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri mbalimbali;

Menejimenti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Tume ya Ulinzi wa taarifa Binafsi;

Viongozi mbalimbali mliopo;

Waheshimiwa Viongozi wa Dini

Wageni Waalikwa,

Waandishi wa Waandishi wa Habari;

Ndugu wananchi;

Wasanii wetu;

Mabibi na Mabwana.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Ndugu zangu, nami niongeze sauti yangu kumshukuru Mungu kutuwezesha kujumuika pamoja katika hafla hii, lakini kutuwezesha kupiga hatua hii muhimu tuliyoifikia leo.

Nitumie pia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa fursa na kunialika kushiriki katika tukio hili leo, wewe na Wizara, nawashukuru, *ahsanteni sana!*

Niishukuru pia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwamba nanyi mpo katika mchakato huu na leo kuna uwepo wa Serikali hapa, nashukuru sana.

Aidha, nikushukuru na kukupongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yako, kwa kazi kubwa mliyoifanya ndani ya kipindi kifupi tangu tulipotunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyounda Tume hii, ambayo leo tunaizindua. Pamoja na kuzindua Tume hii, tayari mmetunga na kuchapisha Kanuni za kutekeleza Sheria hii. **Hongereni sana! kweli nyie ni wadijitali na mambo yenu ni haraka-haraka kidijitali.**

Ndugu zangu

Miaka ya nyuma ila sio nyuma sana, huko duniani, kuna visa vilitokea vilivyohusisha kuvuja kwa taarifa binafsi. Mifano

ni taarifa zinazochukuliwa na hoteli au hospitali kuhusu wateja wao kuvuja na kuleta athari kwa wahusika. Kuna mifano ya kampuni binafsi kutafuta taarifa binafsi za watu kinyume cha haki za watu ili watumie taarifa hizo kwa maslahi yao ya kibiashara. Pia kuna mifano kuhusu vitendo vibaya vilivyowahi kufanywa na watu na vikundi visivyo vyema kudukua mifumo ya taasisi zinazokusanya taarifa binafsi.

Pindi haya yakibainika yanaonesha ukiukwaji wa haki za watu ambao taarifa binafsi zao zimetumiwa ndivyo sivyo. Haya yote yalisababishwa na udhibiti hafifu wa mifumo ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa taarifa binafsi katika taasisi mbalimbali zilizokusanya na kutumia taarifa binafsi. Katika kukabiliana na yote haya, ndio maana tupo hapa leo kuzindua Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Kama ilivyosemwa hapa kabla, kupitia video na wasemaji mbalimbali, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweka bayana kulindwa kwa haki za binadamu na miongoni mwa haki za binadamu ni haki ya kulinda **faragha**. Kwa mujibu wa Ibara ya 16(1) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafasi yake, maisha yake binafsi na familia yake.**

Aidha, Ibara ya 16 (2) ya Katiba ilizitaka Mamlaka za Nchi kuweka utaratibu wa kisheria wa namna ya kulinda haki ya faragha nchini. Kwa upande mwingine, Ibara ya 12 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 linayataka Mataifa kuweka utaratibu unaohakikisha mtu yeyote haingiliwi katika faragha yake, familia yake, nyumbani au kwenye makazi yake wala kuvunjiwa heshima, utu na hadhi yake.

Kwa upande wa kikanda, suala la ulinzi wa haki ya faragha limepewa kipaumbele katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya SADC kupitia miongozo mbalimbali. Umoja wa Afrika nao kupitia Mkataba wa Malabo wa mwaka 2014 unasisitiza ulinzi wa faragha. Kwa ujumla, Jumuiya hizo za Kikanda zinazitaka Nchi Wanachama kulinda uhuru wa faragha kwa kutunga Sheria kubwa tatu ambazo kama alivyosema Waziri ni **Sheria ya Makosa ya Mtandao (the Cybercrime Law); Sheria ya Miamala ya Fedha ya Kielektroniki (the Electronic Transaction Law) na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (the Personal Data Protection).**

Mwaka 2015 nchi yetu ilitunga Sheria mbili kati ya hizo tatu zinazopendekezwa na Jumuiya za Kikanda yaani, Sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Miamala ya Fedha ya

Kielektroniki, hizo tulishazitunga. Hivyo, tulibakiza kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, lakini kama mnavyooona tumeshafanya kazi hiyo na leo tunazindua Tume. Hivyo, kupitia Ilani ya CCM 2020-2025 Chama kiliahidi kuongeza faragha na usiri wa taarifa za wananchi katika mawasiliano kwa **kukamilisha kutunga sheria ya kuimarisha ulinzi wa taarifa na takwimu. Ahadi hii tuliitimiza mwaka 2022, kama ilivyoelezwa hapa.**

Hivyo basi, kufuatia kutungwa kwa Sheria hiyo na leo tunapozindua Tume hii, iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria tajwa ili kulinda haki na maslahi ya raia wetu, sio tu tunatekeleza matakwa ya Katiba yetu bali pia tunatekeleza ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na kukamilisha wajibu wetu kikanda na kimataifa. *Niseme kwamba, hatuna deni, tumekamilisha!*

Ndugu Wananchi,

Kila mwanadamu ana utashi na anastahili staha. Hivyo, zipo baadhi ya Taarifa ambazo asingependa zijulikane kwa kila mtu. Na kwa kweli, ingekuwa taarifa zetu zoote ziko wazi na watu wanazijua, tusingetazamana usoni, au hii dunia ingekuwa ya aina nyingine, hakuna faragha, hakuna staha. Lakini kwa

sababu kila mwanadamu anahitaji staha, anahitaji faragha, ndio maana tumekuja na Sheria hii, ili kutunza utu wa mwanadamu.

Ndugu zangu, zipo baadhi ya taarifa zinazoweza kutumika kuhujumu jamii nzima na wakati mwingine kusababisha unyanyapaa katika jamii. Kwa mfano, Daktari aliyekosa uadilifu akitoa taarifa za ugonjwa wa mtu, aidha ugonjwa wa kurithi au ugonjwa mwingine, inaweza kuleta unyanyapaa kwa familia hiyo. Pengine ni ugonjwa wa kurithi wa familia nzima, akitoa taarifa ya mtu mmoja tu, familia nzima ikawa inanyanyapaliwa. Lakini vilevile unaweza ukatoa taarifa ya mtu, na hiyo taarifa ikaleta vurugu kwenye jamii, vita pengine na mauaji. Kwa hiyo kulikuwa na kila haja ya kuwa na Sheria hii na kuunda Tume hii, ambayo leo tunaizindua.

Kwa kuzingatia maendeleo makubwa ya kiteknolojia, taarifa binafsi za watu zinaweza kukusanywa, kuchakatwa na kutumika bila hata wahusika kufahamu. Ni mara ngapi tunasikia taarifa za mtu zimetoka, tena taarifa halisi, zimechakatwa na kutumika, sasa hiyo haikuwa sawa. Licha ya uwezekano wa taarifa binafsi kutumika kwa hujuma, lakini pia taarifa binafsi ni biashara kubwa kwa makampuni mbalimbali

ya kimtandao. Kwa hiyo hatuna budi kulindana ili tusitumike hivyo.

Kutokana na uhalisia huo, Serikali imelazimika kuweka utaratibu wa kisera na kisheria ili kulinda taarifa binafsi za Watanzania zinazokusanywa, kuchakatwa, kuhifadhiwa na wakati mwingine kusafirishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi na taasisi imara ya usimamizi wa ukusanyaji na uchakataji wa taarifa hizo, ni nyenzo muhimu katika kujenga uchumi na mifumo ya kidigitali. Na hapa niseme, leo tunapozindua Tume hii, Tume itambue kwamba ina kazi nzito sana, na hii ni Tume muhimu sana kwa maisha yetu ya kijamii, kisiasa lakini pia kiuchumi. Mifumo iliyotajwa na Waziri inafika mitano au sita, yote hii mnakwenda kuifuatilia, na yote hiyo inaweza kutumika kiuchumi, kisiasa, wanaotafuta mamlaka wakatamia mifumo hiyo kisiasa, wakawasema wengine, wakapenya. Kwa hiyo usalama wetu kisiasa, kijamii na kiuchumi uko mikononi mwenu. Mwenyekiti wa Tume, Mkurugenzi Mkuu na watumishi wa Tume, maisha yetu yako mikononi mwenu. Heshima zetu ziko mikononi kwenu.

Kama ilivyosemwa hapa, kiuchumi, Tume hii inakwenda kuvutia mitaji kuleta nchini, na mambo mengine ya kukuza *digital inclusive economy* itakwenda kufanywa hapa. Wajibu wa Tume umesemwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri na sitaki nirudie, lakini nitoe maelekezo yafuatayo;

- i. Kwanza,** Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ihakikishe Taasisi zote za umma na binafsi zinazopaswa kusajiliwa zinasajiliwa na kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kabla au ifikapo mwezi **Disemba, 2024**. Taasisi nyingi kama sio zote ziwe tayari zimesajiliwa.
- ii. Pili,** taasisi zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi zihakikishe zinazingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Na niitake Tume kutoa elimu kuisitiza wajibu wa taasisi hizo.
- iii. Tatu,** maafisa wa Tume, Data protection officers, na Tume mna kazi kubwa ya kufanya. Ninataka muifanye kwa weledi na ubora zaidi. Nyinyi ni wadhibiti, lakini zaidi nyinyi ni wawezeshaji. Nendeni mkafanye uwezeshaji ili watoa huduma mbalimbali waridhike na utunzaji wa haki binafsi nchini.

- iv. **Nne**, Mheshimiwa Waziri, hii ni taasisi mpya na jukumu jipya kwa Wizara yako. Kwa upande wa Sera, hakikisheni mnafuatilia kwa karibu kazi za Tume. Fuatilieni kwa karibu ili malalamiko yanayoibuliwa yashughulikiwe kwa haki. Nitapenda Wizara iniletee taarifa ya utekelezaji mara mbili kwa mwaka ili tujue mwenendo tunakwenda vipi. Lakini hapahapa niseme, Mkurugenzi Mkuu wa Tume hii ni Polisi, Mwenyekiti wa Bodi pia ni Polisi pia, kwa hiyo tunategemea kuona utendaji wa haki, na mambo yote yanakwenda kama vile mafunzo yenu ya kipolisi yalivyo.
- v. **Mwisho**, baada ya kuwa na mfumo wa kisera na kisheria wa kulinda taarifa binafsi, **sasa ninaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie na kuhakikisha** mifumo ya TEHAMA yote nchini inasomana kama ninavyosema kila mara. Mifumo yetu lazima isomane, sio kila mtu anachukua njia yake. Ifikapo tarehe **31 Disemba, 2024 mifumo yote ya Serikali iwe inasomana**. Hivyo basi Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wengine na hasa Makatibu Wakuu, nendeni mkasimamie hili liwezekane. Sababu nyinyi mkiweka mguu chini, Waziri hafanyi kitu. Lakini Makatibu Wakuu

mkitaka, mkiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara husika, haya mambo yanawezekana. Naomba sana mkashirikiane kufanya.

Jingine ninalotaka kusema ni kwamba, kuna Taasisi muhimu ziko maeneo mbalimbali, NIDA iko Mambo ya Ndani, EGa iko Utumishi na Tume hii iko Habari, hivyo basi kuwe na mratibu ambaye yuko kati (*neutral*), kwamba Taasisi zote ambazo zinakuwa maeneo mbalimbali zinakuwa regulated. Kaangalieni Sheria zilizounda Taasisi hizi nyingine na ya kwenu muone namna mnavyoweza ku *harmonize* katika kurekebisha sheria zenu ili kuhakikisha kazi yenu inakwenda vizuri.

Baada ya kusema hayo, niwapongeze tena sana kwa hatua hii ambayo mmefikia, matumaini yetu ni makubwa kwenu, tunaiangalia Tume inafanya nini, lakini tunamuangalia Waziri yale mambo uliyosema pale, kwamba Tume itafanya, tunaisubiri kwa hamu. Ndani ya mwaka mmoja, tuanze kuona matokeo. Nihitimishe kwa kushukuru tena kwa kunipa heshima ya kushiriki tukio hili na sasa nipo tayari kuzindua mfumo huu, lakini nimepewa kazi nyingine ya kutoa vyeti kwa Taasisi zilizosajiliwa. Niko tayari kufanya kazi hizo!

Ahsanteni kwa kunisikiliza.